**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

**BARAZA LA SANAA LA TAIFA (BASATA)**


# FOMU YA UHAKIKI WA NYIMBO

**Taarifa za wimbo**

1. **Jina la msanii**: Rapcha
2. **Jina la wimbo**: YEEH
3. **Jina la Mtozi**:Yogo Beats
4. **Tarehe ya Kutoka:**08/09/2024

**Daraja la wimbo**

| WW (U) | WM13(U13) | WM16(U16) | WZ18 (A) | MM (SS) | KK (R) | X |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | ✓ | |

**Moani ya Mhakiki**

Kulingana na Kanuni za Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA), video ya wimbo wa msanii Rapcha yenye jina *YEEH* imepewa Daraja KK sawa na R. Hii inamaanisha kuwa kazi hii ya sanaa imekataliwa na hairuhusiwi kutumika kwa namna yoyote ile.

Sababu ya uamuzi huu ni kwamba maudhui ya video husika ikiwemo mavazi, yaliyowasilishwa yamekiuka mwongozo wa maadili. Ili kazi ya sanaa kama hii iweze kukubalika na kutumika, haitakiwi kuchochea vitendo vya ngono wala kudhalilisha utu wa mtu mwingine.

**ANGALIZO:**

Video ya wimbo huu isiendelee kusambazwa wala kutumika kwenye vyombo vya habari na ushushwe mara moja kwenye mitandao ya kijamii hadi vipande vyenye ukakasi vitakapoondolewa.

Digitally Signed By Kevin M Stansilaus
Mon Sep 08 13:12:53 EAT 2025

Kevin M Stansilaus

**K/MKURUGENZI MSAIDIZI, MUZIKI**


Jengo la Utumishi, 8 Barabara ya Kivukoni, S. L. P 4779, Dar es Salaam, TANZANIA,Simu: +255 738 259 611/481,

Barua Pepe: km@basata.go.tz /info@basata.go.tz, Tovuti: www.basata.go.tz

## NYIMBO ZILIZOTOKA NA KUHAKIKIWA MWEZI WA 12, 2024 PAMOJA NA MCHANGANUO WA KANUNI YA 25 NA MADARAJA

### MCHANGANUO WA KANUNI YA 25.

Kanuni ya 25 Kifungu cha 6 Inaeleza kuwa Ili wimbo uweze kukubalika na kupelekwa kwenye jamii unatakiwa uwe na vitu vifuatavyo

a) Hauvunji heshima ya mwimbaji, msikilizaji na mtazamaji.

b) Hauna upotoshaji wa aina yeyote.

c) Hauchochei ghasia ya aina yoyote au namna yoyote.

d) Hauna meneno ya uongo, uchochezi au yanayo kashifu watu wengine.

e) Hauudhurishi lugha chafu na matusi,

f) Hautukuzi ubaguzi wa rangi, ukabila au dini.

g) Haukashifu Taifa la Tanzania au mataifa mengine.

h) Haudhoofishi umoja, ushirikiano na ustawi bora wa jamii.

i) unazingatia masharti ya sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika masuala ya haki za ubunifu na mambo mengine yote.

j) Haishawishi wala kuhamasisha vitendo vya ngono, ushoga, usagaji au matumizi ya dawa za kulevya.

**MCHANGANUO WA MADARAJA YA KAZI ZA SANAA YA KAZI ZA SANAA**

| Na. | DARAJA | UMRI WA HADHIRA WANAO RUHUSIWA | MAELEZO |
|---|---|---|---|
| 1. | “WW” sawa na “U” | Watu wote | - |
| 2. | “WM 13” sawa na “U13” | Watoto wa kuanzia umri wa miaka 13 na kuendelea. | - |
| 3. | “WM 16” sawa na “U16” | Watoto sawa na umri wa kuanzia miaka 16 na kuendelea. | - |
| 4. | “WZ18” sawa na “A” | Watu wa umri kuanzia miaka 18 na kuendelea. | - |
| 5. | “MM” sawa na “SS” | Maonesho maalum | Maonesho ya kielimu au mafunzo. |
| 6. | “KK” sawa na “R” | Kukataliwa kazi ya Sanaa Pamoja na matumizi yake kwa namna yoyote | Kazi ya Sanaa haitaruhusiwa kusambazwa kwa namna yoyote. |
| 7. | “X” | Hairuhusiwi kuoneshwa mahali popote nchini | Muhusika atakamatwa na kuchukuliwa hatua za kisheria. |